- Awe tayari kutoa mawazo yake kwa lengo la kuwezesha shughuli za huduma kuwa endelevu
- Awe na mzigo moyoni mwake wa kufanikisha shughuli za huduma ikiwa ni pamoja na kuleta watu wengine wenye nia ya kufanikisha shughuli za huduma

## Msisitizo

Mtu yeyeto anaweza kujiunga na huduma hii kwa hiyari yake mwenyewe endapo anawiwa moyoni mwake katika kufanikisha malengo ya huduma kwa njia ya mali zake. ***Mtu yeyote anaweza kuchangia kufanikisha shughuli za huduma bila kuwa Mshirika wa kudumu***.

## Uendeshaji wa Huduma

Huduma ina viongozi waliochaguliwa na wana wajibu wa kutoa taaarifa mbalimbali za maendeleo ya huduma ikiwa ni pamoja na kiasi cha pesa zilizochangwa, majina ya wachangiaji pamoja na kuonesha namna fedha zilivyotumika katika shughuli za huduma. Viongozi pia ndio watiasaini katika uchukuaji fedha kutoka kwenye akaunti ya huduma kwa ajili ya shughuli stahiki.

**Viongozi wa huduma ni**:

1. Mkurugenzi
2. Katibu
3. Mtunza hazina

### Jinsi ya Kutambua Maeneo ya Kujenga Makanisa

Kama ilivyoelezwa hapo awali, huduma hii inahusika na ujenzi wa makanisa maeneo ya vijijini na siyo mijini. Kutokana na ufinyu wa rasirimali fedha, hata huko vijijini bila shaka huduma hii haiwezi kujenga makanisa kila eneo kwa wakati mmoja. Hivyo basi, uongozi wa huduma ya Tujenge Nyumba ya Mungu umeweka vigezo kadhaa ili kurahisisha zoezi la ubainishaji wa maeneo ya kufanyika baraka ya kujenga makanisa. Pamoja na msaada wa mwongozo wa Roho Mtakatifu, vigezo hivyo hutumika kuongoza timu ya wajumbe walioenda kutembelea maeneo husika. Maamzi ya kuchagua eneo la ujenzi hufanywa na timu ya wajumbe hao kisha kushirikisha viongozi wa huduma na baadaye hushirikisha washirika wote juu ya maamzi yao.